

## TANGAZO

### BODI YA KOROSHO TANZANIA

#### FURSA ZA UWEKEZAJI KWA NJIA YA UBIA



Bodi ya Korosho Tanzania (Bodi) ni taasisi ya Umma iliyopewa jukumu la kudhibiti na kusimamia tasnia ya korosho nchini kuanzia uzalishaji, uongezaji wa thamani pamoja na masoko. Aidha sheria ya Tasnia ya Korosho imeruhusu Bodi kuratibu na kusimamia shughuli za kilimo, uwekezaji, Biashara na miradi ya maendeleo yenye manufaa katika ustawi wa tasnia ya korosho. Hivyo Bodi inapenda kutangaza fursa za uwekezaji kwa njia ya ubia zilizopo kwenye tasnia ya korosho. Aidha, Uwekezaji huo utafanyika kwa kuzingatia sheria ya tasnia pamoja na miongozo na sera ya Uwekezaji ya Ubia inayoratibwa chini ya Bodi.

**1. Fursa zinazotangazwa ni kama ifuatavyo:**

- i. Uwepo wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya uongezaji wa thamani wa zao la korosho katika Kongani la viwanda lililopo kijiji cha Maranje, Kata ya Mtiniko Halmashauri ya Nanyamba katika Mkoa wa Mtwara. Iengo la uanzishwaji wa kongani hili la viwanda ni kutekeleza malengo ya Serikali ya kubangua korosho zote zinazozalishwa hapa nchini ifikapo mwaka 2030. Kongani hilo la Viwanda lina ekari 1,572 ambapo eneo la ekari 354 tayari limeshaandaliwa kwa shughuli za uwekezaji na lina miundombinu muhimu kiwemo barabara, umeme, maji nk,
- ii. Uwepo wa Viwanja viwili Mkoani Mtwara vilivyopo jirani na ufukwe wa Bahari ya Hindi (*Beach plots*) kwa ajili ya ujenzi wa ghala au kiwanda; Maeneo haya yapo mkabala na bandari ya Mtwara. Hivyo ni maeneo ya kimkakati kwa uwekezaji wa ghala kwa ajili ya hifadhi ya mazao, pembejeo na shughuli za viwanda. Aidha, yapo maeneo mengine yanayofaa kwa shughuli za makazi na biashara.
- iii. Uwepo wa maeneo kwa ajili ya uanzishaji wa mashamba makubwa ya pamoja (*block farms*) katika mikoa ya Pwani, Lindi na Mbeya.

- iv. Aidha, Bodi inayo maeneo katika jiji la Dar es Salaam yanayofaa kwa ujenzi wa ofisi na shughuli za uzalishaji mali.

## **2. Vigezo vya kuwekeza katika maeneo ya ubia na Bodi ya;**

- i. Kurejea tangazo la Bodi la maeneo yanayotarajiwa kuendelezwa kwa njia ya ubia.
- ii. Muombaji kuwasilisha pendekezo la mradi anaotarajia kuwekeza katika eneo husika, akieleza aina ya mradi tarajiwa, rasimu ya michoro, wigo wa mradi, makadirio ya gharama, mipango ya utekelezaji na gharama, uendeshaji na mapato tarajiwa;
- iii. Mwombaji atawasilisha nyaraka za usajili wa kampuni yake inayoomba kuwekeza kwa njia ya ubia;
- iv. Bodi itajiridhisha kwa kufanya upekuzi unaostahili (*due diligence*) kwa muombaji ili kubaini hali yake ya kisheria, ustadi wa kiufundi, uwezo wa kifedha na taarifa nyingine zozote muhimu zinazohusiana na uwezo wake wa kutekeleza kikamilifu mradi unaopendekezwa;
- v. Bodi itapitia nyaraka za miradi zilizowasilishwa na kufanya maamuzi kulingana na sera yake ya uwekezaji katika miradi ya ubia;
- vi. Bodi itaingia mikataba ya ubia na makampuni au taasisi zilizosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania; na
- vii. Mwekezaji atatakiwa kuweka Dhamana ya Uendelezaji (*Development Bond*) baada ya kusaini mkataba kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi kwa mujibu wa makubaliano yatakayofikiwa.

### **MAWASILIANO**

OFISI YA MKURUGENZI MKUU,  
BODI YA KOROSHO TANZANIA,  
74 BARABARA YA TANU,  
S. L. P 533,  
**63104 MTWARA.**  
Barua pepe; [info@cashew.go.tz](mailto:info@cashew.go.tz)

*Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana na Katibu wa Kamati ya uwekezaji ndugu Jasper Kiwia kwa simu Na; 0693300936*